**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU BUNDA**

**MKOA WA MARA**

**Simu**: 028-2621028

**Fax:** 028-2621028

**Simu** : 0756-066361/0621079460

Baruapepe:bundatc@gmail.com

S.L.P 01,

BUNDA- MARA,

**TANZANIA**.

KUMB.Na.BUNDA/TC/GF/VOL.II /43/111.

04/ 06/ 2026

**Bw /Bi: ..................................................................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA CHUO**

**(JOINING INSTRUCTION) 2026/2027.**

Uongozi wa chuo unafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kozi ya **Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi Mchepuo wa Sayansi ya Jamii na Lugha ya Kiswahili (Kwa kutumia Lugha ya Kiswahili)** miaka miwili (2) au Stashahada ya ualimu Elimu Msingi miaka mitatu hadi minne (3-4) kwa njia ya Masafa.

Kwa mwanachuo wa bweni unatakiwa kufika chuoni kuanzia tarehe **17/08/2026 hadi** tarehe **31/08/2026.** Baada ya tarehe tajwa hapo juu hutapokelewa na kusajiliwa. Ni vema uwahi ili usipoteze nafasi yako hii adimu pia upate maelekezo ya msingi katika mafunzo kabilishi (**orientantion**) kwa ajili ya kujua mambo mbalimbali ya kufuata na kuzingatia katika kipindi chote cha mafunzo kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za chuo.

## 1. MAELEZO MAFUPI KUHUSU CHUO:

Chuo kilianzishwa mwaka 1983 katika wilaya ya Bunda mkoa wa Mara. Bunda ni mahali pazuri na chuo chetu ni kizuri sana. Moto au kauli yetu ni **"HEKIMA NA UMOJA". Dira ya Chuo chetu ni "Kuwa Taasisi ya mfano katika kutoa huduma za kielimu zinazokubalika kwa wateja"**

Chuo kipo umbali wa km 2 kutoka Bunda mjini pembezoni kulia mwa barabara kuu iendayo Musoma/Tarime katika eneo liitwalo **Nyasura**. Shuka katika kituo cha mabasi kiitwacho **Nyasura Stendi** ili kuepuka usumbufu chukua usafiri wa pikipiki ambao ni Tsh 1000/=.

CamScanner

**2. Mahitaji kwa ajili ya usajili ni kama ifuatavyo:**

- Cheti halisi cha kidato cha nne, cheti cha kidato cha sita na cheti cha Ualimu kwa waliohitimu Ualimu nganzi ya cheti (GATCE) na **nakala moja kwa kila cheti**
- **Score sheets / hati ya matokeo yoyote** haitapokelewa isipokuwa kwa **wahitimu ambao vyeti vyao havijatoka**
- Cheti cha kuhitimu shule (**school leaving certificate**).
- Barua hii ya kukuita chuoni (**Joining instruction**).
- Kitambulisho cha shule au kitambulisho kingine kinachokutambulisha kama vile kitambulisho cha kazi, kitambulisho cha taifa (NIDA) au **"passport" au cheti cha kuzaliwa.**
- Aliyeajiriwa awe na kitambulisho cha kazi na barua ya ruhusa toka kwa mwajiri wake ya kumruhusu kuja masomoni.

**3. MALIPO YA ADA NA MICHANGO YA CHUO.**

- **ADA.**

Ada ya mafunzo kwa mwaka ni. Tsh **450,000**/=. Fedha hii italipwa kupitia **Control number** inayotengenezwa katika ofisi ya Mhasibu wa chuo au ofisi ya Usajili.

- **MICHANGO**

Michango inayopaswa kulipwa ni sh. 150,000/=. Fedha hii italipwa kupitia akaunti ya chuo, Miscellaneous **Account 30103500086** NMB BUNDA.

Michango hiyo ni kama ifuatavyo.

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ulinzi | Tsh 30,000/= | kwa mwaka |
| 2. Ukarabati | Tsh 25,000/= | kwa mwaka. |
| 3. Usafi na Mazingira | Tsh 20,000/= | kwa mwaka. |
| 4. Huduma ya kwanza | Tsh 10,000/= | kwa mwaka. |
| 5. Michezo | Tsh 30,000/= | kwa mwaka. |
| 6. Kukodisha godoro | Tsh 10,000/= | kwa mwaka. |
| 7. Serikali ya wanachuo | Tsh 5,000/= | kwa mwaka. |
| 8. Usajili na kitambulisho | Tsh 20,000/= | kwa mwaka wa kwanza tu. |
| 9. Bima ya Afya | Tsh 50,400/= | kwa mwaka. |



CamScanner

ZINGATIA

- Unatakiwa kulipa fedha ya Ada baada ya kupata control namba kutoka ofisi ya **Mhasibu au Usajili** kisha kukabidhi risiti ya benki ( **Bank pay-in- slips**) kwa uthibitisho wakati wa usajili. Piga simu ya Mhasibu namba 0756439917 au Msajili namba 0742050457/0757695078 kwa ajili ya kutengenezewa Control Number.
- Malipo ya Michango yote ya chuo yafanyike kwenye Miscellaneous Account: **No.30103500086 NMB Bunda.** Akaunti tajwa ni kwa ajili ya Malipo ya **michango** tu na si vinginevyo. Malipo yafanyike kwenye tawi lolote la **NMB** kulingana na maelekezo yaliyopo kwa kila mchango kisha utatakiwa kukabidhi risiti ya benki (Bank **pay-in- slips**) kwa uthibitisho wakati wa usajili.
- Wakati wa kulipa hakikisha kwenye risiti ya benki (**Bank pay- in- slips**) linaandikwa jina la mwanafunzi kama lilivyo katika vyeti vyake vya taaluma vya sekondari.
- Kama una bima ya Afya ya (NHIF) **usilipe** huo mchango wa bima ya Afya, njoo na kadi yako ya bima ya afya ya NHIF.
- Tafadhali usifanye malipo yoyote kama hauna ufaulu wa daraja la I, II na III (division I, division II na division III kidato cha sita au hujafaulu Ualimu ngazi ya cheti (GATCE).
- Malipo ya mafunzo kwa njia ya masafa ni kama ifuatavyo: Ada ni Tsh 450,000/=, michango Tsh 150,000/= na ada ya maombi ya kujiunga na mafunzo Tsh 5,000/=.

## 4. SARE YA WANACHUO

Utatakiwa kushona nguo maridadi nadhifu yenye kuonesha haiba nzuri ya Ualimu kama ifuatavyo:

- **WANAUME/WAVULANA.**
  - Suruali moja ya kitambaa chenye rangi ya Dark blue na koti lake kisichoteleza (**Suti)** na Suruali moja ya kitambaa chenye rangi nyeusi na koti lake kisichoteleza (Suti). Suruali zisiwe za kubana bali ziwe nchi "16" chini kwenye miguu
  - Shati moja ya rangi ya zambarau mpauko yenye mikono mirefu na shati moja ya rangi ya light blue (bluu bahari) ambazo ***zinapatikana chuoni.***
  - Tai mbili ambazo ni za rangi ya dark blue na rangi nyeusi.
  - Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vinavyofunika miguu visiwe na visigino virefu.
  - T- shirt moja yenye nembo ya chuo. ***Hii inapatikana chuoni kwa Tshs. 20,000/=***.



CamScanner

➢ **WANAWAKE / WASICHANA.**

- Sketi moja ya kitambaa chenye rangi ya Dark blue na koti lake kisichoteleza (Suti) na Sketi moja ya kitambaa chenye rangi nyeusi na koti lake kisichoteleza (Suti) Shona Linda boksi Inchi 7 kuvuka magoti. Sketi isiwe na mpasuo. Min Sketi haziruhusiwi hapa chuoni.

- Shati moja ya rangi ya zambarau mpauko yenye mikono mirefu na shati moja ya rangi ya light blue (bluu bahari) ambazo ***zinapatikana chuoni***.

- Tai mbili ambazo ni za rangi ya dark blue na rangi nyeusi.


- Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na Kamba vinavyofunika miguu na visivyo na visingino virefu.

- Michoro iliyopo hapo chini inaelekeza jinsi ya kushona Sketi na Suruali.


- T-shirt moja yenye nembo ya chuo. ***Hii inapatikana chuoni kwa Tshs* 20,000/=**

**<u>NB:</u>** Kwa wanachuo wa kike wa kiislamu wanatakiwa kushona hijabu yenye mfanano na rangi ya shati ya chuo ambayo ni rangi ya zambarau mpauko.

(Picha No.01 Sketi na Picha no.02 suruali)



*SKETI YA LINDA BOKSI LA MBELE*



*SURUALI*

**5. MAVAZI YA MICHEZO:**

Michezo ni sehemu ya maisha hapa chuoni. Hivyo wanachuo wote hamna budi kushiriki kikamilifu katika michezo.

Kila mwanachuo anapaswa kuja na vifaa vifuatavyo vya michezo

- Viatu (Raba).



CS CamScanner

- T-shirt na bukta yake ya rangi nyeupe ya Real Madrid ambazo ***Zinapatikana chuoni.***
- Track suti ya rangi ya bluu bahari (light blue) ambayo ***Inapatikana chuoni.***
- Wasichana wanatakiwa kuwa na sketi fupi ya kuvalia juu ya bukta.

**6. VIFAA MUHIMU VYA KUJA NAVYO CHUONI.**

Kwa wasichana na wavulana mnatakiwa kuja na fedha kwa ajili ya manunuzi ya vifaa hivi:-

- ❖ Shuka mbili moja ya rangi ya laiti bluu na moja ya rangi ya pinki kwa ajili ya kujifunika na kutandika, neti moja na blanketi.
- ❖ Picha (03) passport size za rangi kwa ajili ya rekodi za ofisi ya usajili na uadili. Picha ioneshe uso kwa mbele, masikio yote mawili na iwe na background ya rangi ya bluu.
- ❖ Ndoo, sahani, kikombe, bakuli na kijiko kwa matumizi binafsi. ***Vinapatikana chuoni.***
- ❖ Fagio moja aina ya chelewa (yenye mpini). ***Unapatikana chuoni.***
- ❖ Vifaa vya usafi ambavyo ni Mopper rubber (Squizeer) na hardbroom moja. ***Vinapatikana chuoni.***
- ❖ Kumbukumbu za kila siku (portifolio) mafaili (12) na bahasha kubwa moja kwa ajili ya kutunzia vyeti. ***Zinapatikana chuoni.***
- ❖ Ream ya karatasi mbili (02) quire 4 aina ya (double A) yenye jarada la rangi ya bluu. ***Zinapatikana chuo kwa Tsh 20,000/=***

**7. KOZI ZINAZOTOLEWA NA CHUO.**

i STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI MCHEPUO WA SAYANSI YA JAMII NA LUGHA YA KISWAHILI (KWA KUTUMIA LUGHA YA KISWAHILI).

ii STASHAHADA YA UALIMU ELIMU MSINGI KWA MIAKA MITATU HADI MINNE (3-4) KWA NJIA YA MASAFA.

**8. MAELEKEZO MENGINE**

- ❖ Ili kuthibitisha kwamba afya yako ni njema kwa ajili ya mafunzo haya inakupasa upimwe katika Hospitali ya serikali ya Wilaya, Mkoa, Rufaa au Hospitali Teule.
- ❖ Hairuhusiwi kuleta majiko, hita, friji, tv au vifaa vya kielektroniki vya umeme isipokuwa simu ya mkononi.
- ❖ Utasajiliwa na jopo la wakufunzi ambao watahakikisha kila ulichoagizwa umeleta usipokuwa navyo hautapokelewa.
- ❖ Kila mzazi anapaswa kumfungulia mwanachuo anayeripoti chuoni akaunti katika benki ya NMB kama Mwanachuo hajafikisha umri wa kufungua akaunti afunguliwe akaunti ya watoto (Junior Account). Akaunti ifunguliwe kwa Jina sawa na lile lililoko kwenye vyeti vya taaluma vya kidato cha nne na kidato cha sita vya Mwanachuo.

**UONGOZI WA CHUO CHA UALIMU BUNDA UNAKUTAKIA SAFARI NJEMA KUJA CHUONI**

**KARIBU SANA.**

**Mwita Venance Mancheye**
**Mkuu wa chuo**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU BUNDA
S.L.P 1 BUNDA



CamScanner

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

TO: The Medical Officer

From: ..............................
Teachers' College.

.............................................
.............................................

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1. (a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy
2.Neuroses
3.Other serious diseases.
B: Blood Group

Date : ...........................

Signature...............................
Official Stamp

**************************************************************************

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time teacher Education course.

- (a) Eye – sight..........................................................................
  (b) Hearing..........................................................................
  (c ) Limbs..........................................................................
  (d) Speech..........................................................................
  (e) Leprosy..........................................................................

II. Neuroses..........................................................................
III. Other serious diseases..........................................................................
IV. pregnancy..........................................................................

**Date:.............................................Signature..................................**
**Official Stamp**



CS CamScanner

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU BUNDA**

## SHERIA ZA CHUO

Kwa kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imevikabidhi Vyuo vya Ualimu dhamana ya kuwaandaa Wanachuo kuwa Walimu na kuwaendeleza Walimu waliokazini: Sheria hizi zinatoa mwongozo wa kufuatwa ili kufanikisha malengo hayo. Nazo ni:

1. **SHERIA ZA NCHI:**
   Kila Mwanachuo anatakiwa afuate sheria zote za Jamhuri ya Muungano Tanzania kikamilifu. Ni kosa kisheria kuvunja sheria za nchi. **Hivyo utachukuliwa hatua kwa kufuata sheria za nchi.**
2. **ALAMA ZA TAIFA.**
   Kila mwanachuo anatakiwa kuheshimu alama zote za Taifa. Mfano Bendera ya taifa, wimbo wa Taifa. Ni kosa kisheria kutoheshimu alama za Taifa hivyo utachukuliwa hatua za kisheria na kutafukuzwa chuo.

3. **HESHIMA:**
   Waheshimu watumishi wote wa Chuo cha Ualimu Bunda, viongozi, Wageni na Wanachuo wenzio hapa Chuoni na nje ya Chuo. Unyanyasaji wa kila aina hautavumiliwa kabisa. Tunza amani na usalama wa Chuo. Ukipigana na kunyanyasa mwanachuo mwenzako utachukuliwa hatua za kinidhamu au utafukuzwa chuo.

4. **MASOMO/RATIBA.**
   Masomo na shughuli zote zilizopangwa katika ratiba ni muhimu. Kila Mwanachuo anawajibika kufuata ratiba ya chuo kwa kuwahi na kuhudhuria vipindi vyote na kuonyesha bidii ya hali ya juu katika kila somo. Utaondolewa masomoni kwa uzembe wa kutohudhuria masomo darasani na paredi. Kosa la kutozingatia ratiba unaweza kusimamishwa masomo au kufukuzwa chuo.

5. **MALI YA UMMA:**
   Kila mwanachuo anawajibu wa kutunza majengo na vifaa vyote vizuri: Tumia vifaa vizuri na viweke katika hali ya usafi na usalama. Wizi wa aina yoyote ni marufuku kabisa. Mwanachuo atakayebainika amefanya tendo la wizi, kupoteza au kuharibu kifaa chochote cha chuo atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa pamoja na kulipa kifaa hicho au kufukuzwa chuo.

6. **JUHUDI NA MAARIFA.**
   Kila Mwanachuo anapaswa kutumia juhudi na maarifa katika masomo, kazi za nje zote zinazofanywa chuoni na michezo. Uvivu na uzembe hautavumiliwa.

7. **USAFI:**
   a) Chuo kina sare maalum, kila Mwanachuo anapaswa kuvaa sare hiyo wakati wote wa masomo na nje ya chuo
   b) Jiweke katika hali ya usafi kila wakati, aidha yaweke majengo na mazingira ya chuo katika hali ya usafi wakati wote kwa kufanya usafi wa kufagia, kufyeka, kupanda miti,



CamScanner

nyasi na mau. Mwanachuo atakayeonesha tabia ya kutofanya usafi atachukuliwa hatua za kinidhamu au kufukuzwa chuo.

8. **MIKUTANO NA MAWASILIANO:**

a) Mikutano, tafrija, michezo yote hapa chuoni ni lazima ijulikane rasmi kwa Mkufunzi wa zamu, Mwadili na Uongozi wa Chuo ili kibali kitolewe kabla.

b) Mikutano au michezo baina ya wanachuo na Jumuiya ya nje ya Chuo lazima taarifa yake itolewe mapema kwa Mkuu wa Chuo kabla ya kufanyika ili kupata kibali maalum.

c) Mazungumzo yote ya faragha yafanyike mahali pa wazi na siyo kwenye maficho au mahali pa giza.

d) Barua zote za shughuli au Kiofisi ni lazima zipitie kwa Mkuu wa Chuo. Pia taarifa za dharura kuhusu msiba, ugonjwa, n.k. zinazokuja kwa wanachuo lazima zijulikane kwa Mkuu wa chuo

e) Simu za mkononi haziruhusiwi kutumika katika vyumba vya madarasa, mitihani, katika mikutano ya chuo na katika shughuli zote rasmi za Chuo.

**NB:** ***Mwanachuo atakayevunja kipengele chochote hapo juu kati ya "a" hadi "e" atachukuliwa hatua za kinidhamu au kufukuzwa chuo.***

9. **ULEVI NA UVUTAJI SIGARA:**

Ni kosa kuwa katika hali ya ulevi wa aina yoyote. Pombe na madawa ya kulevya ni marufuku kwa wanachuo. Hili ni kosa la kukufukuza chuoni.

10. **MATEMBEZI/RUHUSA:**

a) Matembezi nje ya Mji wa Bunda ni lazima yapate kibali maalum kutoka kwa Mwadili au Mkuu wa chuo.

b) Ruhusa zote za kulala nje ya Chuo na kuwa nje ya Chuo usiku ni lazima zipate kibali cha Mkuu wa Chuo.

c) Wanachuo wa kike ni marufuku kuingia katika mabweni ya wanaume. Pia wanachuo wa wanaume ni marufuku kuingia katika mabweni ya wasichana bila kibali cha mwadili.

d) Hairuhusiwi kutembelea nyumba za Wakufunzi au za Wafanyakazi wengine wa Chuo bila idhini maalumu kutoka kwa mwadili.

e) Wanachuo wakiwa nje ya Chuo ni marufuku kuingia sehemu za kuuzia pombe, mabaa, nyumba za kulala wageni na sehemu nyingine zinazofanana na hizo.

f) Mwanachuo anatakiwa awe chuoni wakati wote wa muhula, ruhusa ya kutoka nje kwa shida maalum hutolewa na Mkuu wa Chuo.

g) Zitakuwepo "Roll Call" kwa wanachuo wote kila siku ili kuhakikisha kuwa mwanachuo yuko kituoni. Pia zitakuwepo rekodi za mahudhurio kwa kila shughuli zilizo katika ratiba.

**NB:** ***Mwanachuo atakayevunja kipengele chochote hapo juu kati ya "a" hadi "g" atachukuliwa hatua za kisheria na kufukuzwa chuo.***

11. **WAGENI:**

a) Wapokee wageni wote wafikao chuoni kwa heshima na ukarimu. Wageni wa Wanachuo hawatakaribishwa chuoni baada ya saa 12:00 jioni na siku za masomo.

b) Mwanachuo apataye mgeni lazima atoe taarifa kwa Mkufunzi wa Zamu au Mwadili mara mgeni afikapo na aondokapo.



CamScanner

c) Wageni wote lazima waandikishwe katika kitabu maalumu cha wageni wa Wanachuo. Wageni waje siku na saa za mapumziko tu.

d) Hairuhusiwi mgeni yeyote kupelekwa mabwenini.

e) Hairuhusiwi kupeleka chombo cha moto mabwenini

12. **UAMINIFU.**

Uwe mzalendo, mvumilivu, mwenye haki; mwaminifu na mkweli katika jambo lolote utendalo na usemalo. Udanganyifu, Uchochezi na Uzushi havitavumiliwa. Hili ni kosa la kusimamishwa masomo au kufukuzwa chuo.

13. **AFYA ZA WANACHUO:**

Kila Mwanachuo anapaswa kuwa na afya njema/timamu. Aidha, kila mmoja anapaswa kujihadhari na vitendo vyovyote vinavyoweza kusababisha maambukizo ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI na magonjwa ya zinaa. Mwanachua atakayebainika anasambaza magonjwa atafukuzwa chuo.

14. **MAHUSIANO YA KIMAPENZI**

Ni marufuku kwa mwanachuo kujihusisha na tabia au mambo yafuatayo;

- Kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanachuo mwenzie au mlezi wake hali ambayo inapelekea kushuka kwa nidhamu na kiwango chake kitaaluma. Mwanachuo atakayevunja sharti hili atafukuzwa chuo.
- Mwanachuo hatakiwi kuwa mjamzito katika kipindi chote cha mafunzo yake. Mwanachuo atakayevunja sharti hili atafukuzwa chuo.
- **Pia ni marufuku kujaribu kutoa mimba au kushiriki kutoa mimba kwa vyovyote vile**. Ukibainika utakamatwa na kupelekwa polisi kwasababu ni kosa la jinai.

15. **PICHA ZA UTUPU**

Ni marufuku kwa mwanachuo **kupiga, kuonesha au kusambaza picha au video za utupu** kwa mwanachuo mwenzake au kwa mtu yeyote. Ukikutwa na kosa la namna hiyo adhabu yake ni kufukuzwa chuo.

**Mwita Venance Mancheye**
**Mkuu wa Chuo**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU BUNDA
S.L.P 1 BUNDA

**NAKALA:**
Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
S .L. P. 10,
**DODOMA.**
Afisa Elimu Wa Mkoa
S.L.P 299
**MARA.**

Mwenyekiti
Bodi ya Ushauri ya Chuo
S.L.P. 01
**BUNDA .**



CamScanner